



Sema mwananchi sema Maoni ya wananchi kuhusu siasa 2015



1. Usuli

Uchaguzi unatoa fursa adimu kwa wananchi kusikika. Viongozi wasiokubalika katika kazi au sera zizizo na ufanisi wanaweza kukataliwa ili kutoa nafasi kwa watu wenye mibadala yenye kuvutia zaidi.

Kwa wakati huu, kampeni za uchaguzi mkuu zinaendelea hapa Tanzania. Mwezi wa kumi mwishoni, wapiga kura watachagua Rais mpya, zaidi ya Wabunge 250 na maelfu kadhaa ya madiwani.

Chama tawala, Chama cha Mapinduzi (CCM) na mgombea wao John Magufuli ambaye ni Waziri wa Ujenzi wanakabiliwa na changamoto mpya ikiwemo vyama kadhaa kuuunda mseto ujulikanao kama Ukawa. Vyama vilivyo ndani ya Ukawa ni:

- Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema)
- Civic United Front (CUF)
- National Convention for Construction and Reform – Mageuzi (NCCR Mageuzi)
- National League for Democracy (NLD)

Mgombea anayewakilisha Ukawa ni Edward Lowassa (aliyewahi kuwa Waziri Mkuu na mwanachama wa CCM).

Vyama vingine vinavyoshiriki uchaguzi bila kuunda mseto ni:

- Alliance for Change and Transparency – Wazalendo (ACT)
- Alliance for Democratic Change (ADC)
- Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA)
- National Reconstruction Alliance (NRA)
- Tanzania Labour Party (TLP)
- United People's Democratic Party (UPDP)

Muhtasari huu umeandikwa na umeandaliwa na Twaweza East Africa.
Umetolewa Septemba 2015

S.L.P. 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301 | uwazi@twaweza.org | www.twaweza.org/sauti



Lakini je, ni masuala gani ambayo yanawagusa zaidi wapiga kura wa Tanzania? Wabunge wametimiza ahadi walizozitoa katika uchaguzi uliopita? Ni vyama gani na wanasiasa gani wanaopendwa au kutopendwa zaidi? Watu wanamtaka nani awe Rais ajaye?

2. Mbinu za utafiti

Tunaweza kushawishika kuchambua masuala kadhaa kwa misingi ya wingi wa watu (nyomi) wanaohudhuria mikutano ya siasa na vichwa vyta habari vinavyochapishwa na waandishi, lakini vigezo hivi vinaweza kuwapotosha wananchi. Kura ya maoni ya wananchi inayoendeshwa kwa ufanisi na umakini inaweza kutoa majibu sahihi zaidi.

Katika muhtasari huu, *Sauti za Wananchi* ya Twaweza, ambayo ni utafiti wa kwanza barani Afrika wenye uwakilishi wakitaifa na unaotumia simu za mkononi, unatoa mambo tisa kuhusu mwelekeo wa kisiasa kwa kutumia takwimu za hivi karibuni kabisa.

Ili kuhakikisha kwamba uchaguzi nasibu unawakilisha vilivyo Tanzania Bara, simu za mkononi na chaja zinazotumia mwanga wa jua ziligawiwa kwa kaya zilizoshiriki. Kaya zisizowakilishwa ni zile tu zilizopo katika maeneo ambayo hayafikiwi na mitando ya simu. (Maelezo zaidi ya mbinu yanatolewa mwisho wa muhutasari huu na kwenye wavuti wa www.twaweza.org/sauti).

Matokeo yanatokana na awamu ya kwanza ya kuwapigia simu wahojiwa wapya 1848. Simu hizi zilipigwa kati ya tarehe 19 Agosti na 7 Septemba 2015. Wakati awamu hii inatekelezwa, kampeni zilikuwa ndo kwanza zimeanza na wiki 8-10 za kampeni zilikuwa zimesalia. Waliopigiwa simu walichaguliwa kwa kutumia mbinu za uchaguzi nasibu zinazotumika na taasisi za utafiti kote Tanzania. Utafiti huu umejumuisha mikoa yote ya Tanzania Bara.

Takwimu hizi zinalinganishwa na zile za awamu za nyuma zikiwemo:

- Utafiti wa awali wa *Sauti za Wananchi* wa mwaka 2012 mwishoni (wahojiwa 2,000)
- *Sauti za Wananchi* Awamu ya 10 kutoka Oktoba 2013(wahojiwa 1,574)
- *Sauti za Wananchi* Awamu ya 24 kutoka Septemba 2014 (wahojiwa 1,445)
- *Sauti za Wananchi* Awamu za utafiti April (wahojiwa 1,316), Mei (wahojiwa 1,335), Juni (wahojiwa 1,335) na Julai (wahojiwa 1,575) 2015 (Kielelezo 4b tu)
- Utafiti mpya wa awali wa *Sauti za Wananchi* wa Julai na Agosti 2015 (wahojiwa 2000)

Katika kila awamu, takwimu zinawakilisha eneo zima la Tanzania Bara. Zanzibar haijashiriki katika tafiti hizi.

3. Mambo tisa kuhusu wapiga kura, masuala ya siasa na wagombea


Jambo la 1: Afya, maji, na elimu ndio changamoto kuu kwa wananchi

Wananchi wanakerwa zaidi na huduma duni za kijamii. Watu 6 kati ya 10 walitaja afya (59%) kuwa ni mionganini mwa matatizo matatu makuu na ukosefu wa maji (46%), elimu duni (44%) (Kielelezo 1). Mwaka huu, watu wengi zaidi walitaja huduma hizi kuliko mwaka uliopita.

Kutoka 2012 hadi 2014, tatizo lililotajwa zaidi lilikuwa umaskini na masuala ya kiuchumi, lakini kwa mwaka huu, tatizo hili liliushuka kutoka 63% hadi 34%.

Hali hii inaweza kuwasaidia wagombea na vyama vyao kuelewa ni wapi wajikite na sera zao ili kushughulikia kero za wapiga kura.

Kielelezo cha 1: Matatizo makuu matatu hapa Tanzania leo ni yapi?
(Asilimia ya majibu yanaonesha ukubwa wa tatizo)



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi*, Utafiti wa Awali (Oktoba–Desemba 2012),
Awamu ya 10 (Oktoba 2013), Awamu ya 24 (Septemba 2014),
Awamu Mpya 1 (Agosti-Septemba 2015)


	2012	2013	2014	2015
Afya	40%	46%	47%	59%
Upatikanaji wa Maji	30%	36%	27%	46%
Elimu	25%	46%	38%	44%
Umaskini / masuala ya kiuchumi	49%	57%	63%	34%
Miundo mbinu	17%	16%	19%	32%
Rushwa / utawala	24%	29%	30%	28%
Usalama duni / taharuki kisiasa	11%	18%	18%	13%
Ukosefu wa ajira	16%	13%	15%	11%
Uhaba wa chakula/njaa kali	20%	7%	12%	9%
Kilimo	13%	13%	8%	5%

Jambo la 2: Wabunge wanatoa ahadi nyingi lakini hawazitekelezi


Wakati wa kampeni za uchaguzi, wagombea wanatoa ahadi kwa wapiga kura. Wananchi walio wengi (64%) wanasema kwamba wanafahamu ahadi zilizotolewa wakati wa kampeni zilizopita (Kielelezo 2a.)

Hata hivyo, wananchi walisema pia kwamba Mbunge wao hakutekeleza ahadi zake. Asilimia 86 walisema kwamba Mbunge wao alitekeleza kidogo au hakutekeleza ahadi kabisa zake. Ni asilimia 8 tu waliosema kwamba Mbunge wao ameteketeleza ahadi zake zilizo nyingi au zote (6%) (Kielelezo 2b.)

Kielelezo cha 2a: Unazijua ahadi zilizotolewa na Mbunge wako ?



Kielelezo cha 2b: Mbunge wako alitekeleza ahadi alizozitoa ?



Chanzo cha Takwimu: Sauti za Wananchi, Awamu ya awali kwa Kundi la Pili (Julai-Agosti 2015)

Jambo la 3: Karibu wananchi wote wanadhamiria kupiga kura katika uchaguzi wa mwaka huu


Mwaka 2010, ni asilimia 43 tu kati ya waliojiandikisha, ambao walipiga kura katika uchaguzi wa Rais. Asilimia hii ni ndogo sana ukilinganisha na uchaguzi wa mwaka 2000 ambapo asilimia 84 walipiga kura na wa mwaka 2005, ambapo asilimia 72 walipiga kura.

Lakini walipoulizwa iwapo walipiga kura mwaka 2010, asilimia 79 walisema kwamba walipiga kura (Kielelezo 3).

Wananchi karibu wote (98%) wanasema kwamba wamejiandikisha kupiga kura na idadi kubwa zaidi (99%) wanasema kwamba wanadhamiria kutumia haki yao ya kupiga kura mwezi Oktoba.

Hata hivyo, ni asilimia 57 tu walioweza kutaja tarehe sahihi ya uchaguzi: 25 Oktoba.

**Kielelezo cha 3: Ulipiga kura mwaka 2010?
Umejiandikisha na unadhamiria kupiga kura mwaka huu?**



Chanzo cha Takwimu: Sauti za Wananchi, Awamu 1 wa Kundi Jipy 1 (Agosti-Septemba 2015)


Jambo la 4: Kwa walio wengi, mchakato wa kujiandikisha ulikuwa na changamoto nyingi lakini walifanikiwa

Zoezi la uandikishaji wa wapiga kura kwa kutumia mchakato mpya wa BVR ultumika ili kuboresha daftari la wapiga kura na kupunguza fursa za wizi wa kura. Mchakato huu ulikuwa mgumu, na wenye changamoto nyingi kupelekea kusitishwa kwake mwanzoni kwa wiki kadhaa baada ya mashine za BVR kuchelewa kufika. Baadaye, mashine zilipofika vyombo vya habari viliripoti malalamiko mengi kuhusu mchakato mzima wa kujiandikisha.

Wananchi walio wengi, walisema walipata au walishuhudia matatizo kadhaa walipoenda kujiandikisha (Kielelezo 4a). Changamoto kuu ilikuwa ni muda uliotumika: wawili kati ya wahojiwa watatu (68%) walisema mistari ilikuwa mirefu na zaidi ya nusu walisema kwamba wengine walitumia zaidi ya masaa sita kujiandikisha.

Watu pia walipata, au waliona, matatizo ya watu kuruka foleni (37%), mashine za BVR kushindwa kufanya kazi kwa usahihi (26%), upendeleo kwenye kituo cha kujiandikisha (19%) au uzoefu finyu wa waliotumia hizi mashine (16%).


Kielelezo cha 4a: Ulipata au kuona matatizo yapi (kama yalikuwepo) wakati wa mchakato wa kuijandikisha kwa kutumia BVR?



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi*, Awamu 1 ya Kundi Jipya 1 (Agosti-Septemba 2015)

Hata hivyo, idadi ya wapiga kura waliojiandikisha ilionekana kuwa nzuri sana. Karibu wote (98%) waloulizwa mwisho wa Agosti na mwanzo wa Septemba walisema kwamba walikuwa tayari wameshajiandikisha. Katika awamu zilizotangulia, asilimia ya walioandikisha ilikuwa chini zaidi. Hata hivyo, asilimia hii ilizidi kupanda wakati wa mchakato wa kuijandikisha (Kielelezo 4b).

Kielelezo cha 4b: Umejandikisha kupiga kura chini ya mpango mpya wa BVR?



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi*, Aprili- Julai 2015,
Awamu 1 ya Kundi Jipya (Agosti-Septemba 2015)

Jambo la 5: CCM ndio chama kinachopendwa zaidi


Sauti za Wananchi iliwauliza wapiga kura jinsi wanavyotegemea kupiga kura za Rais, Wabunge na Madiwani. Na bila kutaja majina ya wagombea, walipanga kupigia kura wagombea wa chama gani?

Kwene nafasi zote (Urais Kielelezo 5a, Mbunge Kielelezo 5b, Diwani Kielelezo 5c), zaidi ya wahojiba 6 katika ya 10 walisema kwamba wanategemea kumchagua mgombea wa CCM.

Wanaowaunga mkono Chadema wamepungua kidogo tangu 2013.


Mwaka 2014, asilimia 16-18 waliripoti kwamba hawatomchagua mgombea kutokana na chama chake bali yeye mwenyewe. Hata hivyo mwaka 2015, hakuna muhojiwa yeyote aliyeripoti hivyo.

Kielelezo cha 5: Uchaguzi ungefanyika leo, ungempigia kura mgombea wa chama gani?




	2012	2013	2014	2015
CCM	61%	47%	51%	66%
CHADEMA	30%	30%	23%	22%
CUF	4%	4%	4%	1%
ACT-WAZALENDO	0%	0%	0%	0%
NCCR MAGEUZI	0%	1%	1%	0%
UKAWA*	0%	0%	0%	3%
CHAMA KINGINE	1%	2%	0%	6%
SIJUI / HAKUNA JIBU	4%	0%	4%	2%

Kielelezo cha 5b: Mbunge




	2012	2013	2014	2015
CCM	60%	44%	46%	60%
CHADEMA	31%	31%	24%	24%
CUF	4%	4%	4%	2%
ACT-WAZALENDO	0%	0%	0%	1%
NCCR MAGEUZI	0%	1%	1%	1%
UKAWA*	0%	0%	0%	3%
CHAMA KINGINE	0%	2%	1%	6%
SIJUI / HAKUNA JIBU	5%	0%	5%	2%

Kielelezo cha 5c: Diwani



	2012	2013	2014	2015
CCM	61%	45%	47%	60%
CHADEMA	29%	30%	23%	26%
CUF	4%	4%	4%	3%
ACT-WAZALENDO	0%	0%	0%	1%
NCCR MAGEUZI	0%	1%	1%	1%
UKAWA*	0%	0%	0%	3%
CHAMA KINGINE	1%	2%	1%	6%
SIJUI / HAKUNA JIBU	5%	0%	5%	2%

Kielelezo cha 5d: Unajisikia uko karibu zaidi na chama gani?



	2012	2013	2014	2015
CCM	65%	54%	54%	62%
CHADEMA	26%	32%	27%	25%
CUF	3%	4%	4%	2%
ACT-WAZALENDO	0%	0%	0%	1%
NCCR MAGEUZI	0%	1%	1%	0%
UKAWA*	0%	0%	0%	2%
CHAMA KINGINE	2%	1%	2%	2%
SIJUI / HAKUNA JIBU	4%	0%	2%	5%

* Ikumbukwe kuwa Ukawa imejumuishwa katika kielezo hiki ilikuonyesha kuwa wananchi wanadhani kwamba Ukawa ni chama. Ukawa haijasajiliwa kama chama cha siasa.

Chanzo cha Takwimu: Awamu ya 10 (Octoba 2013), Awamu ya 24 (Septemba 2014), Awamu 1 ya Kundi Jipya (Agosti-Septemba 2015)

Wahojiwa hawakupatiwa orodha ya majibu ya kuchagua. Hata hivyo, matokeo yote yalirekodiwa na kumbukumbu zilihifadhiwa kwa usahihii. Vyama vyote vilivyopata angalau asilimia 1 katika miaka ambayo utafiti ulifanywa vimejumuishwa kwenye kielelezo.


Jambo la 6: Nafasi rasmi ya Ukawa haieleweki vizuri

Mseto wa vyama vya upinzani, Ukawa (Umoja wa Katiba ya Wananchi, au Walinzi wa Katiba ya Wananchi), unajumuisha vyama vinne vya siasa – Chadema, CUF, NCCR Mageuzi na NLD. Umoja huu uliundwa ili kuwawezesha wanachama kuingia katika uchaguzi huu wakiwa na ilani moja na mgombea mmoja kutoka chama kimojawapo kwa kila jimbo.


Lakini mseto huu haujasajiliwa kama chama cha siasa na jina la ‘Ukawa’ halitakuwepo kwenye karatasi za kupigia kura. Hata hivyo, karibu nusu ya wananchi (49%) wanadhani Ukawa ni chama kama vyama vingine na kwamba kimesajiliwa (Kielelezo 6a). Wengi zaidi (57%) wanategemea kuona neno ‘Ukawa’ kwenye karatasi ya kupigia kura (Kielelezo 6b).

Kuona hivi kunaweza kuongeza hali ya kutokuwa na uhakika kwenye maamuzi ya wapiga kura siku ya uchaguzi itakapowadia. Ni dhahiri kuwa kampeni na elimu kwa wapiga kura hazifanyi juhudhi za kusahihisha wazo hilo lisilo la kweli.

Kielelezo cha 6a: Je Ukawa ni chama cha siasa kilichosajiliwa Tanzania?



Kielelezo cha 6b: Je jina la Ukawa litaonekana kwenye karatasi ya kupigia kura siku ya uchaguzi wa mwaka 2015?




Source of data: Sauti za Wananchi, Awamu 1 ya Kundi Jipya (Agosti 2015)

Jambo la 7: John Magufuli anaongoza kwenye kura ya maoni

Walipoulizwa na *Sauti za Wananchi* wangempigia kura nani iwapo uchaguzi wa Rais ungefanyika siku ya mahojiano, kati ya wahojiwa watatu, wawili (65%) walisema kwamba wangempigia kura John Magufuli, mgombea urais wa CCM (Kielelezo 7a). Robo (25%) walisema wangempigia kura Edward Lowassa, mgombea wa Chadema na mseto wa Ukawa, na ni 3% tu waliosema wangemchagua mgombea mwengine. (7% hawakujua wangemchagua nani, ama walikataa kutaja jina).

**Kielelezo cha 7: Ukimwacha Rais Kikwete,
iwapo uchaguzi wa Rais ungefanyika leo, ungemchagua nani?**



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi*, awamu 1 ya Kundi Jipya (Agosti 2015)
Wahojiwa hawakupatiwa orodha ya majibu ya kuchagua.
Hata hivyo, matokeo yote yalirekodiwa na kumbukumbu zilihifadhiwa kwa usahihi.

Izingatiwe kwamba dodoso la utafiti huu liliandaliwa kabla ya uteuzi wa wagombea urais wa vyama vingine (nje ya mseto wa Ukawa), kikiwemo ACT-Wazalendo.

Aidha, utafiti uliwaauliza watu wangempigia kura nani iwapo uchaguzi ungefanyika siku ileile. Simu hizi zilipigwa kati ya tarehe 19 Agosti na 7 Septemba 2015. Wakati awamu hii inatekelezwa, kampeni zilikuwa ndo kwanza zimeanza na wiki 8-10 za kampeni zilikuwa zimesalia.

Utafiti huu si utabiri wa matokeo ya uchaguzi. Inaonyesha tu kwamba John Magufuli wa CCM alikuwa anaongoza mwanzo wa kampeni.

**Jambo la 8: Jinsia, umri na maeneo wanayotoka wapiga kura hayana
ushawishi mkubwa kwao**

Viwango vya kumuunga mkono John Magufuli na Edward Lowassa vinaweza kuonekana katika makundi mbalimbali ya kijamii.

Magufuli anaungwa mkono zaidi na wanawake kuliko wanaume (68% na 62%) (Kielelezo 8a). Kinyume chake, Lowassa anaungwa mkono zaidi na wanaume kuliko wanawake (28% na 22%).

Halikadhilika, Lowassa anaungwa mkono zaidi mjini kuliko vijijini, wakati Magufuli anaungwa mkono zaidi vijijini kuliko mjini (Kielelezo 8b).

Katika maeneo hayo yote, tofauti kati ya wanawake na wanaume na katika ya wakazi wa vijijini na mijini ni ndogo sana kiasi kwamba hazina maana kitakwimu.


Uwezekano wa vijana (33%) kumpigia kura Lowassa ni mara mbili ya ule wa wazee (15%) (Kielelezo 8c). Magufuli anaungwa mkono kwa wingi zaidi na walio na umri zaidi ya miaka 50 (76%), na kidogo zaidi na vijana (57%).

Watu waliosoma zaidi wanaripotiwa kuelekea kumpigia kura Lowassa mara mbili kuliko wale waliokaa shulenii miaka michache (Kielelezo 8d). Kwa Magufuli hali ni kinyume chake. Anaungwa mkono zaidi na wale wenye miaka michache shulenii kuliko wale waliohitimu sekondari au zaidi.


Hata hivyo, katika vikundi vyote, John Magufuli wa CCM anaonekana kuungwa mkono zaidi kuliko Edward Lowassa wa Chadema na Ukawa.

Kielelezo cha 8: Wafuasi wa John Magufuli na Edward Lowassa katika makundi mbalimbali vya jamii


Kielelezo cha 8a: Wapiga kura wa kike na wa kiume




Kielelezo cha 8b: Wakazi wa vijijini na mijini



Kielelezo cha 8c: Rika mbalimbali



Kielelezo cha 8d: Ngazi ya elimu aliyomaliza



- hawakusoma
- hawakumaliza shule ya msingi
- walihitimu elimu ya shule ya msingi
- hawakumaliza elimu ya sekondari
- walihitimu elimu ya sekondari
- elimu ya chuo kikuu/ufundi

Chanzo cha Takwimu: Sauti za Wananchi, Awamu 1 ya Kundi Jipya (Agosti 2015)

Wahojiwa hawakupatiwa orodha ya majibu ya kuchagua.

Hata hivyo, matokeo yote yalirekodiwa na kumbukumbu zilifadhiwa kwa usahihi.


Jambo la 9: Wafuasi wa John Magufuli wanamuona kama “mchapakazi”, wakati wafuasi wa Edward Lowassa walisema “anaweza kuleta mabadiliko yanayohitajika Tanzania”

Sauti za Wananchi iliwaliza wahojiwa kuhusu vigezo watakavyovitumia kumchagua mgombea Rais.

Upande wa John Magufuli, sifa yake kuu kwa wananchi ni kuwa “mchapakazi”. Asilimia 26 ya wananchi walisema watamchagua kwa sababu hii.

Wafuasi wa Lowassa walisema kwamba ataleta mabadiliko yanayohitajika nchini. Asilimia 12% ya wananchi walisema watampigia kura kwa sababu hii.

Kielelezo cha 9: Kwa nini utampigia kura mgombea huyu?



Chanzo cha Takwimu: Sauti za Wananchi, Awamu 1 ya Kundi Jipya (Agosti 2015)

Asilimia zimehesabiwa kutokana na jumla ya wahojiwa,

na sio wale tu waliompendelea mgombea yeyote.

4. Majumuisho wa matokeo makuu:

- Jambo la 1: Huduma za afya (iliyotajwa na 59%), ukosefu wa maji (iliyotajwa na 46%), elimu duni (iliyotajwa na 44%) na umaskini (iliyotajwa na 34%) ni mambo makuu yanayowakera wananchi, karibu sawasawa na miaka ya nyuma.
- Jambo la 2: Wabunge wanatoa ahadi lakini hawazitekelezi. 64% ya watu wanakumbuka ahadi za uchaguzi uliopita za Mbunge wao na 86% ya watu wanasema kwamba Wabunge wametekeleza ahadi chache kati ya hizo au hawajatekeleza kabisa.
- Jambo la 3: Karibu wananchi wote (99%) wanasema kwamba watapiga kura katika uchaguzi wa mwaka huu lakini ni 57% tu walioweza kuitaja kwa usahihi tarehe ya uchaguzi.
- Jambo la 4: Mchakato wa kujiandikisha uliwasumbua wananchi lakini walifanikiwa (98% wanasema kwamba sasa wamejiandikisha). Tatizo kuu lilikuwa foleni ndefu (68%).
- Jambo la 5: CCM inapendwa zaidi kuliko vyama vingine. Zaidi ya 60% walisema kwamba watamchagua mgombea wa CCM wa Urais, Ubunge na Udiwani.
- Jambo la 6: Nafasi rasmi ya Ukawa haieleweki vizuri. 49% wanafikiri kwamba Ukawa ni chama cha siasa kilichosajiliwa na 57% wanafikiri kwamba jina la ‘Ukawa’ litajitokeza kwenye karatasi ya kupigia kura.
- Jambo la 7: John Magufuli anaongoza katika kura ya maoni. 65% walisema kwamba watamchagua kuwa Rais iwapo uchaguzi ungefanyika siku ya kura ya maoni.
- Jambo la 8: Jinsia, umri na maeneo wanayotoka wapiga kura hayana ushawishi mkubwa katika maamuzi yao. Hata hivyo, makundi yote kwa ujumla yalioneckana kumpenda John Magufuli zaidi.
- Jambo la 9: Wafuasi wa John Magufuli wanamuona kama “mchapakazi”. 26% ya wananchi watamchagua kwa sababu hii wakati wafuasi wa Edward Lowassa wanasema kwamba “anaweza kuleta mabadiliko yanayohitajika nchini”. 12% ya wananchi watamchagua kwa sababu hii.

5. Maelezo kuhusu Mbinu Zilizotumika

Sauti za Wananchi ni utafiti unaokusanya maoni yanayowakilisha wananchi wa Tanzania Bara kwa kutumia simu za mikononi (mobile phone panel survey) (Zanzibar si sehemu ya utafiti huu). Misingi ya mpango huu wa utafiti ni ileile ya tafiti za ana kwa ana na inatumika na taasisi za utafiti zinazoheshimiwa duniani kote.

Utafiti unatumia *random probability sampling*. Maana yake ni kwamba kila mwananchi ana nafasi sawa sawa ya kuchaguliwa katika uchaguzi nasibu. Kundi la wananchi wanaochaguliwa kinasibu (*at random*) inatumika kukadiria wastani wa mgawanyo wa tabia, mtazamo, au maoni ya wananchi wote kwa ujumla. Hii ni njia inayokubalika kisayansi na kura za maoni za siasa kote duniani. Ni njia inaotumiwa na wanatakwimu na wanasyansi wa jamii kuchunguza mwenendo na maoni ya binadamu, iwe katika Ofisi za Takwimu za Taifa, kama vile NBS hapa Tanzania, katika vyuo vikuu na katika makampuni binafsi ya utafiti kama vile *Gallup*, *Pew Research*, na *Ipsos Synovate*.

Kwa ajili ya kundi nasibu ya *Sauti za Wananchi* maeneo mawili ya taarifa, mijini na vijijini, yalibainishwa. Kaya 2,000 ziliundwa katika hatua tatu, kwa kutumia uchaguzi nasibu kwenye kila hatua:

- Maeneo 200 ya kuhesabia (EAs) yalichaguliwa kinasibu kutoka Tanzania Bara yote
- Kaya 10 zilichaguliwa kinasibu kutoka kwenye orodha ya kaya zote katika kila eneo la kuhesabia (EA)
- Mtu mzima mmoja alichaguliwa kinasibu katika kila kaya

Kila kaya ilipewa simu na chaja inayotumia nguvu ya juu. Kila mwezi, wahojiwa walipigwa simu kuhusu mada mbalimbali.

Matokeo katika muhtasari huu yanatokana hasa na awamu ya kwanza ya simu zilizopigwa kwa kundi jipya la wahojiwa 1,848, lililoundwa mwisho wa Agosti na mwanzo wa Septemba 2015. Kwa matokeo hayo ya kura ya maoni '*margin of error ilikuwa ni 2.5%*'. Kwa mfano, tukikadiria kwamba mgombea X anapendwa zaidi na 10% ya Watanzania, tofauti inaweza kuwa kati ya 7.5% na 12.5%. Tuna uhakika wa asilimia 95 kwamba kupendwa kwa mgombea X na wananchi wote wa Tanzania Bara itakuwa ndani ya mipaka hii.

Mambo mengi yatatokea kati ya muda wa kuendesha utafiti huu na uchaguzi mwenyewe mwisho wa Oktoba. Haiwezekani kutabiri matokeo ya uchaguzi kwa uhakika. Takwimu hii ni picha ya mara moja tu ya kiasi cha kupendwa kwa wanasiasa wakati kampeni za uchaguzi zilipoanza. Matokeo haya yatawapatia viongozi picha ya jinsi wapiga kura wanavyowaona kwa wakati huu. Lakini bado kuna fursa nyingi kwa vyama na wagombea amba walipata asilimia ndogo kuwafikia na hata kuwapitia wale wenye asilimia kubwa, na kwa waliopendwa zaidi kushuka katika kupendwa kwao.

Kwa maelezo zaidi, tembelea www.twaweza.org/sauti, ambapo maelezo kamili zaidi kuhusu mbinu za utafiti yanapatikana, pamoja na nyenzo nyingine zikiwemo dodoso na takwimu kamili.